

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam  
23 Februari 2008**

**Waliohudhuria**

Ally Saidi Mwishehe  
Aseli Wilison  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Husein Hamza Hamisi  
Jumanne Idd Selemani  
Kassim Bakari  
Kibwana Mohammad Msiga  
Paulo Atibu Hatibu

**Ofisi**

Ally Saidi Mohammed hakuwepo kwenye mkutano na bado hajaweka ubao wa pili wa tangazo. Wanachama watamkumbusha wakimwona wakati wa wiki.

Mejah alimwambia Elaine kwamba atapaka rangi kwenye milango na nje ya ofisi na nembo na jina la UWABA.

Elaine atasubiri mpaka muda wa ufunguzi wa ofisi unakaribia kabla ya kuprint karatasi nyingi kwa ofisi ziwe safi bila vyumbi siku la ufunguzi.

Juma na Elaine walichukua Tsh 465,000 na waliweka hela hii pamoja na Tsh 35,000 ya hela ya UWABA ambayo walikuwa nayo. Hela hii ilitumikwa na Juma kununua jaketi 30 za njano na ilitumikwa na Mejah kununua helmeti 30 za mitumba. Hela inayobaki inatumikwa na Mejah kutengeneza T-Shirt 30. Zawadi hizi zitatolewa kwa wanachama siku ya ufunguzi.

**Kijarida ya Kali Mata**

Kali Mata, shikira la wanawake wanaotumia baisikeli Gezaulole, walitutumia kwa posta kijarida chao kwa Kiingereza na Kiswahili. Kijarida kilikuwa na repoti ya ushirikiano wa Kali Mata katika Msafara wa Baisikeli ya UWABA. Kijarida ipo ofisini ili wanachama wasome.

**Ben Bikes na Wamba Memorial Fund**

Elaine alienda South Africa kwa likizo, na wakati alikuwepo alikutana na Andrew Wheeldon wa Ben Bikes, shirika ambayo itafanya kazi pamoja na UWABA kwenye mradi wa usalama barabarani kwa kutumia hela ya Wamba Memorial Fund. Pia alitambulisha wafanyakazi na wanaojitolea wengine wa Ben Bikes, alimwonyesha ofisi zao na alimwambia kuhusu miradi yao. Elaine alimwambia kuhusu habari za UWABA. Alitupa nakala ya repoti ya mwaka 2007, na wanachama walipenda kuisoma na kuangalia picha. Wanachama walipenda kupata taarifa zaidi kuhusu shirika lingine ambalo lipo Afrika ambalo lina malengo na miradi kama yale ya UWABA lakini kubwa zaidi.

Bado hatujapata mawasiliano kutoka Wamba Memorial Fund kuhusu vipi tutapata fedha, na Elaine aliwatumia email kuwakumbusha wiki hii.

### **Barabara ya Morogoro**

Baada ya mazungunzo kuhusu Barabara ya Morogoro kwenye mkutano wa nyuma, Elaine aliweka mawazo na mapendekezo wetu kwenye barua na Juma alileta kwa Halmashauri la Jiji kwenye ofisi ya Mama Mlamba.

### **Tawi la Temeke**

Tuliamua tutafanya mkutano wa kwanza wa tawi la Temeke la UWABA jumamosi tarehe 8 Machi saa nne asubuhi Sterio Sokoni Temeke panapopaki maguta. Elaine ataprint vipeperushi kutangaza mkutano huu na Paulo atasambaza kwa wapanda baisikeli kabla ya mkutano.

### **Mashindano ya kuandika hadithi/mawazo**

Ibiki wana mashindano kwa watoto kuandika hadithi au mawazo kuhusu baisikeli. Lazima zifike kabla ya mwezi wa tano. Paulo alileta picha ambazo mtoto mwenye miaka 15 alichora lakini kwa watoto wa umri hii lazima waandike kitu pia. Alisema atahamasisha mtoto kufanya hivi.

### **Mambo ya hela**

Ally Saidi Mwishehe aliendelea kulipa UWABA Tsh 7,000 kila wiki na alileta hela ya wiki hii kwenye mkutano.

Kwenye mkutano wa tarehe 22 Desemba tulikuwa tumekubali na pendekezo la Elaine kumpa Juma posho ya Tsh 20,000 kwa sababu ya kazi nyingi ya UWABA anafanya. Lakini inaonekana tulikuwa na machanganyakio kwa sababu wanachama wengine walielewa hii itakuwa posho ya mara moja tu na wanachama wengine walielewa itakuwa ya kila mwezi. Hussein, Kibwana na Filbert walisema haifai sana kumpa mwanachama moja posho ya kila mwezi wakati wanachama wengine pia wanachangia muda wao. Walipendekeza UWABA tunaweza kutoa posho maalum kila mara kwa mara kwa wanachama ambao wametumia muda nyingi yao kwa ajili ya kazi ya UWABA kama hela inapatikana, lakini hii isiwe posho ya kila mwezi. Wanachama wote walikubali na pendekezo hili.

Hussein alipendekeza kwamba taarifa ya hela ya guta ipatikane kwa urahisi zaidi na tulikubali kwamba kila wiki tutatoa repoti ya hela gani ipo benki na hela gani ya UWABA ipo nyumbani kwa Juma na hela gani imetumikwa wakati wa wiki.